

15/12/2020

**Kumb. Na:** NSS/JIF/2020/.....

Jina la Mwanafunzi:.....

S.L.P.....

**BARIADI**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAKABINDI**  
**WILAYA YA BARIADI MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Nyakabindi ipo umbali wa Km 20 Kaskazini Mashariki mwa Halmashauri ya Mji wa Bariadi barabara kuu iendayo Mwanza kupitia Dutwa pembeni kidogo ya viwanja vya Nanenane Nyakabindi.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** saa moja kamili asubuhi **na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2021** (ndani ya siku saba).

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare za Shule**

- A)** Sare ya Shule hii kwa **Wavulana** ni shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi, viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba pia viwe vya kung'arisha na kiwi na viwe na visigino vifupi(**buti haziruhusiwi**), Soksi jozi mbili rangi nyeusi, Suruali mbili ( moja rangi ya kijivu na nyingine dark blue) zenye turn up chini na zisiwe za kubana(**model**), sweta rangi ya kijani kibichi, Tai mbili (moja rangi ya kijivu na nyingine dark blue) na mkanda mweusi wa wastani(belt ndogo) usio na chata yoyote ile.

Kwa upande wa **Wasichana sare yao ni:** shati mbili nyeupe za mikono mifupi, viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba pia viwe vya kung'arisha na kiwi na viwe na visigino vifupi, Soksi jozi mbili rangi nyeupe, Sketi mbili **ndefu za kuvuka magoti** (moja rangi ya kijivu na nyingine dark blue) na ziwe na malinda makubwa, Sweta kijani kibichi na Tai mbili (moja rangi ya kijivu na nyingine dark blue).

- B)** Rangi ya Hijabu ifanane na Sare za Shule.

- C)** Sare ya michezo kwa Shule hii kwa **Wavulana** ni truck suit ya njano, raba jozi moja, soksi ndefu za njano na Tshirt ya njano pamoja na tshirt ya blue yenye nembo ya shule. Kwa **wasichana** ni Tracksuit ya njano, raba nyeupe, soksi nyeupe na Tshirt rangi ya njano pamoja na tshirt ya blue yenye nembo ya shule.

2.2 Counter books 12 quire mbili au zaidi, kalamu mbili au zaidi na mkebe wa hesabu.

2.3 Chakula kwa wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda Shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

2.4 Mahitaji mengine ya kibinadamu.

### **3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima;
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
- d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa;
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii;
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- i) Kutunza mali za umma.

### **3.2 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule:**

- a) Wizi.
- b) Uasherati na Ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito / kupata mimba/ kusababisha mimba.
- i) Kuo au Kuolewa.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea, na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi.
- n) Udanganyifu katika Mitihani ya aina yoyote ile.

### **4.0 Mambo Mengine Muhimu Yanayopaswa Kukamilishwa na Kuwasilishwa Shuleni na Mwanafunzi:**

- a) 'Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

### **5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**JOSEPH ELIAS  
MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Kiambatisho A: FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA  
WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Anuani ya Mwanafunzi:  
S.L.P.....  
BARIADI

MKUU WA SHULE,  
NYAKABINDI SEKONDARI,  
S.L.P 341-BARIADI.

Mimi.....ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga kidato cha Kwanza mwaka 2021 Nyakabindi Sekondari nakubali kujiunga na shule hii. Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mtiifu, mwadilifu na kuwa nitafuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitatunza mali zote za umma zilizopo Shuleni na nitasoma kwa bidii na uwezo wangu wote nikishirikiana kikamilifu na wanafunzi wenzangu katika kazi zote za Shule iwe za darasani, nje au michezo. Nitaishi kwa amani na kujiheshimu katika jumuiya ya shule na jumuiya inayoizunguka shule. Pia, naapa kuwa sitashiriki katika migomo, fujo yoyote na sitatenda kosa lolote la jinai na ikitokea hivyo hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu ikiwemo adhabu kali pamoja na kufukuzwa shule maramoja.

.....  
SAHIHI YA MWANAFUNZI                      TAREHE                      Mbele ya MKUU WA SHULE

**Kiambatisho B: FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA  
MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

Anuani ya MZAZI/MLEZI:  
S.L.P.....  
BARIADI  
Simu:.....

Mimi.....Mzazi/Mlezi wa.....  
ambaye ni mwanafunzi wa shule ya Sekondari Nyakabindi **naahidi** kuwa:

- (a) Mtoto wangu atafika shuleni na vifaa vyote vilivyoagizwa na shule katika fomu hii.
- (b) Nitashirikiana na jumuiya ya Shule kumsisitiza mwanangu kufuata sheria zote za shule.
- (c) Mtoto wangu awapo nyumbani nitampatia muda na mazingira mazuri ya kujifunzia, kufanya mazoezi aliyopatiwa na walimu wake (home work) na nitamwelekeza pale nitakapoweza.
- (d) Nitawajibika ipasavyo kumpatia mwanangu matibabu pindi anapougua shuleni.
- (e) Sitakubali mwanangu kutohudhuria shuleni siku za masomo bila taarifa ya maandishi kwa uongozi wa Shule. Nitaomba ruhusa kwa walimu endapo kuna tatizo.
- (f) Niko tayari kuchukuliwa hatua kali za kisheria pindi nitakapokiuka kiapo hiki.

.....  
SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI                      TAREHE                      Mbele ya MKUU WA SHULE

## HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI

### FOMU YA KUTHIBITISHA UHALALI WA MWANAFUNZI

*(Fomu hii Ijazwe na Mwl. Mkuu wa shule ya msingi aliyosomea mwanafunzi)*

SHULE YA MSINGI .....

S.L.P. ....

BARIADI.

TAREHE.....

PICHA

Mkuu wa shule,  
Shule ya sekondari Nyakabindi,  
S.L.P. 341,  
**BARIADI.**

Ndugu,

### **YAH: FOMU YA KUTHIBITISHA UHALALI WA MWANAFUNZI ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAKABINDI.**

Mimi (jina kamili).....ambaye ni Mwalimu Mkuu wa  
shule ya Msingi.....

Nathibitisha kuwa, Mwanafunzi.....ambaye  
picha yake imebandikwa hapo juu ni mwanafunzi halali aliyechaguliwa kutoka shule hii  
kujiunga na shule ya sekondari Nyakabindi.

.....  
**Sahihi na Mhuri wa Mwl. Mkuu**

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

### FOMU HII IJAZWE KWA USHIRIKIANO WA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI.....
2. TAREHE YA KUZALIWA .....
3. MVULANA/MSICHANA.....
4. URAIA.....KABILA.....DHEHEBU.....
5. SHULE ALIYOKUWA AKISOMA.....
6. (a) JINA LA BABA.....HAI/HAYATI  
(b) KAZI YAKE..... ANAPOISHI.....  
(c) ANUANI..... SIMU .....
7. (a) JINA LA MAMA.....HAI/HAYATI  
(b) KAZI YAKE.....  
(c) ANAPOISHI (KIJIJI/MTAA).....  
(d) ANUANI.....SIMU.....
8. (a) JINA KAMILI LA MLEZI (KAMA HANA MZAZI)  
.....  
(b) UHUSIANO NA MLEZI.....  
(c) KAZI YAKE.....  
(d) ANAPOISHI (KIJIJI /MTAA).....  
(e)ANUANI .....SIMU.....
9. KATIKA FAMILIA
  - IDADI YA KAKA.....
  - IDADI YA DADA.....
  - YEYE NI WA NGAPI KUZALIWA.....
10. AFYA YAKE (KAMA ANA TATIZO ELEZEA HAPA)  
.....  
.....
  - ❖ MIMI (mwanafunzi).....  
NAAHIDI KUWA NITATII NA KUFUATA AMRI NA SHERIA ZOTE ZA SHULE ZILIZOWEKWA.
  - ❖ MIMI MZAZI/MLEZI WA .....
    - NAKUBALIANA NA KUKIRI SHERIA ZOTE ZA SHULE NITAMSISITIZA MWANANGU KUZIFUATA NA KUZIZINGATIA.
    - AIDHA NINAKUBALIANA NA MAELEZO MENGINE YOTE YALIYOWEKWA.

.....  
**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**

.....  
**SAHIHI YA MWANAFUNZI**

**PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
NYAKABINDI SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

*This form must be completed by a Government Medical Officer*

Student's full name:.....Age:..... Sex:.....

Blood Test.....

Stool Examination.....

T.S Test.....

Asthma.....

Eye Disorder.....

Ear Disorder.....

Nose Disorder.....

Anemia.....

Chest (T.B).....

Operations.....

Serious accidents.....

Any other infection disease.....

Pregnancy (Females only).....

ADDITIONAL INFORMATION (E.g. Physical impairment, Chronic or Family disease requiring special attention/treatment, etc).

.....  
.....

I certify that I have personally examined the above named student and recommend that He / She is fit / unfit to pursue secondary school studies at Nyakabindi secondary school.

Name..... Signature..... Designation.....

Date..... Official rubber stamp.....

